

ASb
approved



Kiswahili


Bahati mbaya!

Brigid Simiyu
Abraham Muzee




Mimi na Kiki ni
marafiki.

Sisi hutembeda
kwenda nyumbani.




Siku moja,
mwanamme
alitufuata.



Meno yake
yalikuwa ya
kutisha.

Ngozi yake ilijaa
vipele.




Tulipomtazama,
alitupigia kelele
kwa hasira.



Yeye na wenzake
walinisukuma
ndani ya gari.



Kiki aliweza
kutoroka.



Waliniweka katika
chumba chenye
giza.

Walinifunga
mikono.



Mwanamme
mmoja alisema,
"Kula chakula hiki.
Safari ni ndefu."



Nilipokuwa nikila,
yule mwanamme
alivuta sigara.



Ghafla, wenzake
walirudi.

Walikuwa
wanamvuta Kiki.



Tuliwasikia
wanaume hao
wakipingana kwa
sauti ya juu.



Kiki alisema,
"Lazima tutoroke.
Wazazi wetu
hawataweza
kuwalipa."



Tulivuta mbao
kutoka kwenye
dirisha.

Tuliona mwangaza.



Kiki alikuwa mdogo
kuniliko.

Alitoka kwenda
kutafuta usaidizi.



Wanaume
waliingia ndani
kwa fujo.

Kiongozi wao
alikasirika sana.



Walirudi katika
chumba
walichokuwa.

Waliendelea
kugombana.



Mara nilisikia sauti
ikisema,
"Usiogope. Polisi
wamefika."



Kulikuwa na kelele
nyingi pamoja na
milio ya risasi.



Polisi wa kike
alisema, "Kila kitu
ni sawa. Uko
salama sasa."



Tangu siku hiyo,
mimi na Kiki
tumekuwa
waangalifu
zaidi.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way:

Bahati mbaya!

Author - Richard Khadambi and Collins Kipkirui

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Abraham Muzee

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

